

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

Simu: 255-262961500/1  
Nukushi: 255-262961502  
Barua pepe : [press@ikulu.go.tz](mailto:press@ikulu.go.tz)  
Tovuti : [www.ikulu.go.tz](http://www.ikulu.go.tz)



OFISI YA RAIS,  
IKULU,  
1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,  
CHAMWINO,  
S.L.P 1102,  
40400 DODOMA.

*Dodoma*  
*1 Agosti, 2024*

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan leo amezindua rasmi Mradi wa Kimkakati wa Reli kwa Viwango vya Kimataifa (SGR).

Katika tukio la kihistoria Rais Dkt. Samia amezindua rasmi huduma za safari za treni ya umeme ya SGR kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma, majengo ya Stesheni za Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma, na miundomboni ya reli kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma yenye urefu wa kilomita 722.

Rais Dkt. Samia ameongoza Watanzania katika uzinduzi huo kwa kusafiri kwa njia ya reli kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma. Aidha, uzinduzi huo ulihitimishwa na hafla ya uzinduzi iliyofanyika katika Stesheni ya SGR ya Dodoma.

Pamoja na mambo mengine, Rais Samia amepongeza mchango wa Marais Wastaafu katika kufanikisha mradi huo utakaoleta mageuzi ya kiuchumi, na amesisitiza kuwa kukamilika kwa vipande vya reli kutoka Dar hadi Dodoma ni utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa inayolenga kujenga Tanzania yenye uchumi jumuiishi.

Kwa upande mwingine, Rais Dkt. Samia ameiagiza Wizara ya Uchukuzi, Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya Shirika la Reli (TRC) kuhakikisha vipande vya reli ya kisasa vinavyoendelea kujengwa kwenda Mwanza na Kigoma vinakamilika kwa wakati na kwa viwango vya ubora uliokubaliwa.

Aidha, Rais Dkt. Samia amesema lengo ni kufanya reli isomane kibiashara na bandari za bahari na Maziwa Makuu na kufungamanisha bandari na usafiri wa anga kwa kuingiza reli katika *Terminal 3* ya Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere.

Vile vile, Rais Dkt. Samia ameitaka Wizara hiyo kuhakikisha ujenzi na ukarabati wa meli za kubeba mizigo unaoendelea kwenye maziwa mbalimbali unakamilika kabla ujenzi wa mradi huu haujaisha.

Akielezea manufaa ya mradi huu wa kimkakati, Rais Dkt. Samia amesema reli hii itaongeza ufanisi wa bandari nchini hususan bandari ya Dar es Salaam kwa

kuondosha mizigo kwa haraka zaidi kutokana na uwezo wake wa kuhudumia shehena ya **tani milioni 17** kwa mwaka.

Rais Dkt. Samia ameongeza kuwa mradi huu utachochea shughuli za kiuchumi, hususan katika sekta za viwanda, kilimo, ufugaji, utalii na biashara na hivyo kukuza sekta ya viwanda katika maeneo mengine ya nchi kutokana na uhakika wa usafiri na usafirishaji. Hivyo, Reli hii itaongeza biashara hapa nchini pamoja na nchi za jirani hususan zile zisizo na bandari pamoja na kikanda.

Reli hii pia itaimarisha biashara kati ya nchi yetu na nchi zinazohudumiwa na Ushoroba wa Kati (*Central Corridor*), zikiwemo Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Rwanda na Uganda na kuchochea ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi

Hali kadhalika, Rais Dkt. Samia ameeleza kuwa Mradi huu pia utapunguza msongamano wa magari barabarani na ajali, kuongeza ufanisi wa usafirishaji wa vifurushi na kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kutumia reli hii hii inayotumia nishati ya umeme.



Sharifa B. Nyanga

Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu